# HAZINA YETU

ISSN: 3108-8597









TOLEO MAALUMU

## ZIARA YA WAZIRI WA FEDHA MKOANI TANGA MWAKA 2026


# TANGA
## Lango Kuu la Uchumi Afrika Mashariki



# MHE. BALOZI OMAR AUMWAGIA SIFA MKOA WA TANGA KWA FURSA LUKUKI ZA KIUCHUMI

Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), amesema kuwa mkoa wa Tanga umekaa kimkakati katika kukuza na kuchangia katika pato la Taifa kutokana na kuwa na fursa nyingi za kiuchumi ikiwemo Bandari ya Tanga, viwanda na sekta ya utalii.

Mhe. Balozi Omar alisema alipokutana kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dkt. Batilda Buriani, katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, siku ya kwanza ya ziara yake ya kikazi ya siku tatu mkoani humo.



Katika mazungumzo yao, Mhe. Balozi Omar alisema Mkoa wa Tanga una nafasi muhimu katika maendeleo ya uchumi wa Taifa kutokana na kuwa lango muhimu la biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na mchango wake mkubwa katika ukuaji wa sekta ya viwanda nchini, kwa kuwa ina fursa zote za kiuwezeshaji ikiwemo Bandari.

Alisisitiza umuhimu wa wananchi kuchangamkia fursa hizo zikiwemo zile zinazotokana na utekelezaji wa Bajeti Kuu ya Serikali zinazohusu kuwawezesha kiuchumi vijana, wanawake na makundi maalumu kupitia mikopo ya Halmashauri, uanzishwaji wa biashara baada ya Serikali kuondoa sharti la kulipa kodi kwa biashara mpya zinazofunguliwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, pamoja na kunufaika na sekta ya ununuzi wa umma.

*Katika Sekta ya ununuzi wa umma tumeweka masharti kwa biashara au kandarasi zote zinazo anzia shilingi bilioni 50 kushuka chini zitawahusu wazawa pekee, hivyo watanzania wachangamkie fursa hizo" alisisitiza Mhe. Balozi Omar.*









Kwa upande wake, Dkt. Batilda Buriani alisema kuwa Mkoa wa Tanga ni mkoa wa kimkakati kwa kuwa una miundombinu muhimu ikiwemo bandari, reli, barabara na nishati ambayo itasaidia Tanzania kufikia azma ya kuwa na uchumi wa dola trilioni 1 ifikapo mwaka 2050.

Aliishukuru Serikali ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuupatia mkoa wa Tanga kiasi kikubwa cha fedha kinachotumika kuboresha miundombinu ya uwekezaji na huduma za wananchi ikiwemo Uwanja wa Ndege wa Tanga, Bandari ya Tanga, barabara, vituo vya afya na elimu na kwamba hatua hiyo imeufungua kiuchumi mkoa huo.

Aidha, Dkt. Batilda alimshukuru Mhe. Waziri kwa kutembelea mkoa huo na kumkaribisha rasmi katika ziara yake, ambayo itahusisha kutembelea shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na miradi inayotekelezwa na Serikali kwa ajili ya wananchi mkoani humo.





# MHE. BALOZI OMAR AIPONGEZA TPA KWA KUONGEZA UFANISI WA BANDARI YA TANGA



Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), ameipongeza Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa kuongeza ufanisi wa Bandari ya Tanga kufuatia uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika kuboresha miundombinu ya bandari hiyo, hatua ambayo imeiwezesha kupokea meli kubwa za mizigo kutoka mataifa mbalimbali duniani na kuongeza mchango wake katika uchumi wa Taifa.

Mhe. Balozi Omar amesema hayo alipofanya ziara katika Bandari ya Tanga kwa lengo la kujionea utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Bandari hiyo, ambapo alieleza kuridhika na mafanikio yaliyopatikana baada ya Serikali kuboresha kina cha Bandari na kujenga gati mpya yenye urefu wa mita 456, ambalo sasa linaruhusu meli kubwa za mizigo kuingia na kutia nanga.

Alisema mafanikio hayo yameifanya Bandari ya Tanga kupokea kwa mara ya kwanza meli kubwa za mizigo zilizotoka moja kwa moja nchini Marekani na China, mataifa yenye uchumi wa kwanza na wa pili kwa ukubwa duniani, jambo linalodhihirisha kuongezeka kwa ushindani na uwezo wa Bandari hiyo katika kuhudumia biashara ya kimataifa.



*Awali kina cha Bandari hakikuruhusu meli kubwa kuingia moja kwa moja.*

*Leo hii, kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali, Bandari ya Tanga imeanza kupokea meli kubwa kutoka Marekani na China moja kwa moja. Haya ni mafanikio makubwa yanayostahili pongezi," alisema Mhe. Balozi Omar.*

Aidha, alieleza kuwa mipango ya Serikali ya kuongeza urefu wa gati kutoka mita 456 hadi mita 900 kwa ajili ya kuhudumia makasha (containers) itaongeza zaidi uwezo wa Bandari ya Tanga na kuiwezesha kuwa kitovu muhimu cha usafirishaji wa mizigo katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mhe. Balozi Omar alisema ongezeko la uwezo wa Bandari hiyo linafungua fursa mpya za uwekezaji kwa sekta binafsi, hususan katika ujenzi wa maghala ya kuhifadhi mizigo na utoaji wa huduma za vifaa vya usafirishaji nje ya eneo la Bandari, huku akiwahimiza wafanyabiashara na wawekezaji wa Mkoa wa Tanga kuzitumia ipasavyo fursa hizo.

*Pamoja na huduma za sasa za usafiri wa abiria kati ya Tanga na Pemba, Serikali itaendelea kuweka mazingira yatakayowezesha Bandari ya Tanga kupokea meli za kitalii (cruise ships), hatua itakayochochea ukuaji wa sekta ya utalii na shughuli nyingine za kiuchumi katika mkoa huu" alisema Mhe. Balozi Omar*




Kwa upande wake Meneja wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) Mkoa wa Tanga, Bw. Salehe Mbega, alisema kuwa uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika upanuzi wa gati na kuongeza kina cha Bandari umebadili kwa kiasi kikubwa uwezo wake ambapo sasa inapokea meli kubwa zinazowasili moja kwa moja (direct call) kutoka mataifa mbalimbali badala ya kutegemea meli ndogo (feeder vessels) kama ilivyokuwa awali.

Bw. Mbega alisema maboresho hayo pia yameongeza kasi ya kuhudumia mizigo kwa kupunguza muda wa kuhudumia meli kutoka wastai  wa siku nane hadi kumi hadi kufikia siku tatu hadi tano, sambamba na kuondoa gharama zilizokuwa zikitokana na uhamishaji wa mizigo kutoka baharini kwenda gatini.

Aidha, amesema idadi ya meli zinazohudumiwa imeongezeka kutoka wastani wa meli 100 kwa mwaka kabla ya maboresho hadi meli 616 katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2026, huku kiwango cha shehena kikiongezeka kutoka takribani tani 500,000 hadi kufikia tani milioni 2.17 kwa mwaka.







Alieleza kuwa Bandari ya Tanga sasa inahudumia pia mizigo mikubwa ya miradi ya kimkakati ya Serikali ikiwemo miradi ya umeme, gesi na Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).





*Maboresho yaliyofanywa yameongeza kwa kiwango kikubwa uwezo wa Bandari ya Tanga, kiasi kwamba ndani ya miaka miwili hadi mitatu tu tumeanza kushuhudia ongezeko kubwa la meli na shehena kuliko tulivyotarajia.*

Hali hiyo imeifanya Bandari kuanza kufikia ukomo wa uwezo wake, ndiyo maana tunaendelea na mpango wa awamu inayofuata wa upanuzi wa gati tatu na kuongeza maeneo ya kuhifadhi mizigo kwa kushirikiana pia na sekta binafsi kupitia bandari kavu (dry ports)," alisema Bw. Salehe Mbega.





Katika Ziara hiyo Mhe. Balozi Omar aliambatana na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Dkt. Batilda Buriani, Mkuu wa Wilaya ya Tanga Mjini, Mhe. Dadi Kolimba, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambaye pia ni Mhasibu Mkuu wa Serikali, CPA Leonard Mkude, Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bw. Mcha Hassan Mcha, na Makamishna na maafisa waandamizi kutoka Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake.


CROWN
MEDIA
JAMBO





# WAFANYABIASHARA WAHIMIZWA KUONGEZA MAUZO NJE YA NCHI ILI KUPUNGUZA NAKISI YA BIASHARA

Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), ametoa wito kwa wafanyabiashara, wawekezaji na wazalishaji nchini kuongeza uzalishaji wenye tija na kuimarisha mauzo ya bidhaa katika masoko ya kimataifa ili kupunguza nakisi ya biashara (trade deficit) na kuongeza mchango wa sekta ya biashara katika kukuza uchumi wa Taifa.

Akizungumza wakati alipotembelea Kituo cha Huduma ya Pamoja Mpakani cha Horohoro, mkoani Tanga, ikiwa ni sehemu ya ziara yake mkoani humo, Mhe. Balozi Khamis alisema pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika ukusanyaji wa mapato na uboreshaji wa mazingira ya biashara, bado ipo haja ya kuongeza thamani ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi ili Tanzania iweze kunufaika zaidi na biashara ya kimataifa.

Mhe. Balozi Omar alieleza kuwa takwimu za biashara kupitia Kituo cha Forodha cha Horohoro zinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha uliopita bidhaa zenye thamani ya takribani shilingi bilioni 748 zilipitia katika kituo hicho, lakini kati ya hizo, bidhaa zilizouzwa nje ya nchi zilikuwa na thamani ya takribani shilingi bilioni 238 pekee, wakati bidhaa zilizoingizwa nchini zilifikia thamani ya shilingi bilioni 510, hali inayoonesha kuwepo kwa nakisi kubwa ya biashara.

"Matarajio ya kila taifa ni kuuza bidhaa nyingi zaidi kuliko linazoagiza kutoka nje, Takwimu hizi zinatuonesha bado tuna kazi kubwa ya kufanya katika kuongeza uzalishaji na kuimarisha mauzo ya bidhaa zetu nje ya nchi na Tanga ina fursa nyingi za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa, hivyo ni muhimu kuzitumia kikamilifu ili kupunguza nakisi hii," alisema Mhe. Balozi Khamis.

Alisisitiza kuwa Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara kupitia uwekezaji katika miundombinu ya forodha, mifumo ya kisasa ya ukaguzi wa mizigo pamoja na kuimarisha vituo vya mipakani ili kurahisisha biashara na kuongeza ushindani wa bidhaa za Tanzania katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Aidha, alisema mafanikio ya ukuaji wa uchumi yanatoa msingi mzuri wa kuongezeka kwa shughuli za biashara nchini, akibainisha kuwa uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.3 mwaka 2026, jambo litakalochochea ongezeko la uzalishaji na biashara.

Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, Mhe. Balozi Khamis alisema Kituo cha Huduma ya Pamoja Mpakani cha Horohoro, kimewekewa lengo la kukusanya shilingi bilioni 136 katika mwaka wa fedha 2026/27, baada ya kuvuka matarajio ya mwaka uliopita kwa kukusanya shilingi bilioni 125, hivyo kutokana na mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi na biashara, Serikali ina imani kuwa lengo hilo litafikiwa, huku akibainisha kuwa kituo hicho kinachangia karibu robo ya mapato yote yaliyopangwa kukusanywa katika Mkoa wa Tanga.





*Serikali imetenga shilingi bilioni 573 katika Bajeti ya mwaka 2026/27 kwa ajili ya kuendeleza maboresho ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ikiwemo ununuzi wa scanners (midaki) 27 za kisasa zitakazowekwa katika vituo mbalimbali vya forodha nchini, ikiwemo Kituo cha Forodha cha Horohoro" alisema Mhe. Balozi Omar*

Alieleza kuwa mchakato wa ununuzi wa vifaa hivyo tayari umeanza na unafanyika kwa kuzingatia taratibu zote za ununuzi wa umma, huku akieleza kuwa vifaa hivyo hutengenezwa kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya kila kituo cha forodha, hivyo mchakato wake unahusisha usanifu, utengenezaji, ukaguzi wa ubora, usafirishaji na ufungaji kabla ya kuanza kutumika na uwekezaji huo utaongeza ufanisi wa ukaguzi wa mizigo, kuharakisha utoaji wa huduma, kuimarisha usalama wa mipaka na kuongeza usahihi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

*Hatununui tu vifaa vya kisasa, bali tunawekeza katika kuongeza ufanisi wa biashara, kuimarisha usalama wa nchi na kuhakikisha Serikali inapata mapato yake stahiki, ma Midaki hii itasaidia kujua kwa uhakika bidhaa zinazopita mipakani, kupunguza muda wa ukaguzi na kurahisisha biashara halali," aliongeza Mhe. Balozi Omar.*





Aliwahimiza pia wafanyabiashara kuendelea kutumia Kituo cha Huduma ya Pamoja Mpakani cha Horohoro, kufanya biashara halali na kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje, akisisitiza kuwa hatua hiyo itaongeza mapato ya fedha za kigeni, kupunguza nakisi ya biashara (trade deficit) na kuimarisha uchumi wa nchi.

Naye Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tanga ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga mjini, Mhe. Dadi Kolimba, alisema Mkoa wa Tanga unaendelea kuwa miongoni mwa mikoa inayoongoza nchini katika ukusanyaji wa mapato, ukiwa wa sita kitaifa, mafanikio ambayo yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na utendaji mzuri wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na ushirikiano wa taasisi nyingine za Serikali zinazofanya kazi katika vituo vya mipakani.

Alisema Kituo cha Forodha cha Horohoro ni miongoni mwa vituo muhimu vya kiuchumi vinavyochangia kwa kiwango kikubwa mapato ya Mkoa wa Tanga na Taifa kwa ujumla, akibainisha kuwa katika mwaka wa fedha uliopita kituo hicho kilivuka lengo lake kwa kukusanya shilingi bilioni 125 dhidi ya lengo la shilingi bilioni 115.

Aliongeza kuwa Serikali ya Mkoa itaendelea kushirikiana na TRA kutatua changamoto zinazojitokeza, kuimarisha mazingira ya biashara na kuhamasisha uzalishaji pamoja na mauzo ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya nje ili kuongeza mapato ya Serikali na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kwa Upande wao Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Bw. Mcha Hassan Mcha, na Afisa Mfawidhi wa Kituo cha Huduma ya Pamoja Mpakani cha Horohoro, Bw. Shadrack Mbonea, walisema kuwa wamejipanga vyema kupambana na Magendo kwa kuimarisha doria za kimkakati kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali.



# MHE BALOZI OMAR: SERIKALI KUENDELEA KUBORESHA HUDUMA ZA KIJAMII

SERIKALI imeahidi kutoa shilingi Milioni 750 ili kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyosalia katika Kituo kipya cha Afya Kange, kilichopo katika kata ya Maweni, jijini Tanga, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuboresha huduma za afya kwa wananchi katika kata hiyo.

Ahadi hiyo imetolewa leo na Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb) wakati wa ziara yake ya kikazi jijini Tanga ambapo alikagua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Kituo cha Afya Maweni , mradi wa mabweni katika Shule Kongwe ya Sekondari Usagara na Mradi wa Ukarabati wa Shule Kongwe ya Msingi Funguni Wilaya ya Pangani.

Aliwataka wakazi wa mkoa huo kufuata maelekezo ya wataalam wa afya kupunguza maradhi kwa kutunza mazingira, kuchemsha maji ya kunywa, kusafisha maeneo ya makazi ili kuua vimelea vinavyosababisha maradhi ikiwemo kipindupindu na kwa wale watakao ugua basi wakitumie kikamilifu Kituo hicho cha Afya Kange.

"

*Baada ya kuwasilishwa kwa maombi ya fedha za kukamilisha ujenzi wa Kituo hiki na uongozi, nimenong'ona na Mstahiki Meya wa Jiji la Tanga na Mkuu wa Wilaya na baada ya majadiliano yao wamenieleza kuwa zinahitajika shilingi milioni 750, ili majengo yote yakamilike na kuanza kutoa huduma kwa wananchi, nitawasiliana na mkoa, Halmashauri ya Jiji na Wizara ya Fedha ili kiasi hicho kipatikane na kukamilisha ujenzi" alisema Mhe. Balozi Omar.*



Mhe. Balozi Omar alisisitiza umuhimu wa wananchi kukitunza kituo hicho cha afya ili kiweze kuwafaa kwa muda mrefu.

Aidha, Mhe. Balozi Omar alibainisha kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026, Serikali imejitahidi kuweka kwa kiasi kikubwa cha fedha katika Mkoa wa Tanga kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo.












*Kwa mwaka huu wa fedha uliopita, Mkoa wa Tanga ulipangiwa kutumia Shilingi bilioni 528.1, na Serikali imewasilisha kiasi cha shilingi bilioni 487.5. Sawa na ufanisi wa asilimia 92 ya fedha zote zilizopangwa kutolewa," alisisitiza Mhe. Balozi Omar.*

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Mhe. Dadi Kolimba, aliishukuru Serikali, kwa kuipatia Wilaya yake kiasi cha shilingi bilioni bilioni 350 zilizoelekezwa kuekekeza miradi mbalimbali ya maendeleo na huduma za wananchi katika kipindi cha miaka 5 iliyopita.




# WANAFUNZI WAASWA KUJIKITA KWENYE MASOMO ILI KUJENGA MAISHA YAO YA BAADAYE

Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), amewataka wanafunzi nchini kutumia ipasavyo fursa ya elimu wanayoipata kwa kujikita katika masomo yao, akisisitiza kuwa elimu ndiyo msingi wa mafanikio ya mtu binafsi na maendeleo ya taifa.

Rai hiyo aliitoa wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa Bweni la wanafunzi wavulana wa kidato cha tano na cha sita katika Shule ya Sekondari ya Usagara mkoani Tanga.

Mhe. Balozi Omar alisema jukumu kuu la mwanafunzi ni kusoma kwa bidii na kujiandaa kwa maisha ya baadaye.

> "*Jukumu la wanafunzi ni kusoma, huu ndiyo muda wenu wa kujifunza na kujiandaa kwa maisha yenu ya baadaye. Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia, walimu wanatoa maarifa na wazazi wanatimiza wajibu wao wa kuwalea na kuwahudumia. Kilichobaki kwa wanafunzi ni kufanya bidii katika masomo yenu", alisema Mhe. Balozi Omar.*

Alibainisha kuwa Serikali inaendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwa kuboresha miundombinu ya shule, ikiwemo ujenzi wa mabweni, madarasa na huduma nyingine muhimu zinazochochea ufaulu wa wanafunzi.


Alisema mabweni yana mchango mkubwa katika kuongeza muda wa kujifunza, kuimarisha nidhamu na kuboresha matokeo ya mitihani, ndiyo maana Serikali imeendelea kuyapa kipaumbele katika shule mbalimbali nchini.

Mhe. Omar aliwapongeza walimu wa Shule ya Sekondari ya Usagara kwa kazi nzuri ya kuwalea na kuwafundisha wanafunzi, akiwataka kuendelea kujituma ili kuongeza kiwango cha ufaulu na kuandaa wahitimu wenye maarifa na maadili mema.

Alieleza kuwa kukamilika kwa bweni hilo kutawawezesha wanafunzi wengi zaidi kuishi shuleni, kupunguza muda wanaotumia kutembea kwenda na kurudi nyumbani na kuongeza muda wa kujisomea, jambo litakalosaidia kuinua zaidi kiwango cha ufaulu wa shule hiyo kongwe.

Katika kuunga mkono jitihada hizo, Mhe. Omar aliahidi Serikali kutoa shilingi milioni 37 kwa ajili ya ununuzi wa vitanda ili bweni hilo lianze kutumika hususani kwenye sakafu ya chini ambayo imekamilika.

Bweni hilo la ghorofa tatu linajengwa kwa ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Halmashauri ya Jiji la Tanga na litakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 240 wa kidato cha tano na sita.




WAZIRI WA FEDHA











# SERIKALI KUFUATILIA KWA KARIBU MRADI WA BARABARA PANGANI HADI TANGA YENYE UREFU WA KM 50

Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), amesema Serikali itafuatilia kwa karibu changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Pangani-Tanga ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi pamoja na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi.

Mhe. Balozi Omar alitoa kauli hiyo alipotembelea mradi wa ujenzi wa sehemu ya barabara ya Pangani mkoani Tanga yenye urefu wa kilometa 50 kwa kiwango cha lami, ambayo ni sehemu ya mradi mkubwa wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge)–Saadani–Pangani yenye urefu wa kilometa 256.

Ziara hiyo inafuatia kilio cha uongozi wa mkoa na Wilaya ya Tanga pamoja na wakazi wa Wilaya ya Tanga wanaoathirika na ubovu wa barabara hiyo unaokwamisha shughuli zao za kiuchumi hususan wakati wa mvua na masika.

Alisema mradi huo umechelewa kukamilika kwa muda mrefu, hali inayolazimu Serikali kuangalia kwa kina changamoto zinazouchelewesha ili kuhakikisha unakamilika na wananchi wanaanza kunufaika na huduma za usafiri na usafirishaji.





*Mradi huu ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi na uchumi wa nchi. Tutafuatilia changamoto zinazoukabili ili utekelezaji wake ukamilike kwa wakati na uweze kutoa huduma iliyokusudiwa," alisema Mhe. Balozi Omar.*

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara nchini-TANROADS Mkoa wa Tanga, Bw. Jotrevas August, alisema kuwa Mkandarasi anasuasua kukamilisha mradi licha ya juhudi za Serikali kuwataka watekeleze ujenzi wa mradi huo kwa wakati.



Aidha, ujenzi wa madaraja pamoja na matengenezo ya barabara ya awali na ya mchepuko kwa kiwango cha changarawe unaendelea sambamba na hatua nyingine za utekelezaji wa mradi.

Bw. August alisema kuwa mradi huo utakuwa kiungo muhimu kinachounganisha Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mombasa, hatua itakayoongeza ufanisi wa biashara na usafirishaji katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mradi wa barabara ya Bagamoyo (Makurunge)–Saadani–Pangani unatarajiwa kuwa moja ya miundombinu muhimu ya kimkakati itakayorahisisha usafiri, kuimarisha biashara na kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika ukanda wa pwani na nchi jirani za Afrika Mashariki.





MCCC Ltd








# WAZIRI WA FEDHA AWAPONGEZA WAFANYABIASHARA KWA KULIPA KODI MKOANI TANGA

Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), amewapongeza wafanyabiashara wa Mkoa wa Tanga kwa ushirikiano wao katika kutekeleza wajibu wa kulipa kodi, akibainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Tanga ilivuka lengo la makusanyo kwa asilimia 26.

Mhe. Balozi Omar ametoa pongezi hizo wakati akizungumza na Wafanyabiashara wa Mkoa wa Tanga wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo, ambapo alisisitiza kuwa  ulipaji wa kodi ni msingi muhimu wa maendeleo ya Taifa na unachangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali.

Alisema kuwa makadirio ya ukusanyaji wa kodi kwa mwaka huo yalikuwa shilingi bilioni 425.74, lakini  TRA ilikusanya

shilingi bilioni 535.79 kutokana na ushirikiano mzuri wa wafanyabiashara na walipakodi.

*TRA ndiyo inayokusanya kodi, lakini wafanyabiashara ndiyo wadau wakuu na mawakala muhimu wa maendeleo kupitia ulipaji wa kodi. Serikali inathamini mchango wenu katika kujenga uchumi wa taifa," alisema Mhe. Balozi Omar*



Aidha, alisema Serikali imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 580 kutoka Mkoa wa Tanga katika mwaka wa fedha 2026/2027, akiwataka wafanyabiashara kuendelea kulipa kodi kwa hiari na kwa uaminifu kulingana na shughuli wanazozifanya.

Mhe. Omar alisisitiza kuwa takribani theluthi mbili ya mapato ya Serikali yanapaswa kugharamiwa na kodi za ndani ili kuiwezesha Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo bila kutegemea misaada ya nje.

Alisema kuwa wafanyabiashara wanapofanikiwa Serikali pia inapofanikiwa, kwa kupata mapato yanayowezesha kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi na kuwekeza katika miundombinu ya maendeleo.

Aidha, alisema kuwa Serikali imeendelea kuwekeza na itaendelea kuimarisha miundombinu ya Bandari ya Tanga na Forodha ili kuongeza ufanisi wa shughuli za biashara, kuvutia uwekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Tanga na nchi kwa ujumla.

Aliongeza kuwa Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC), ikiwemo kuongeza mabehewa ya mizigo ili kuongeza ufanisi wa biashara na kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya usafirishaji.

Alisema kuwa Mkoa wa Tanga una fursa nyingi za kiuchumi na umeendelea kuwa tulivu licha ya changamoto mbalimbali zinazolikabili dunia, hali inayowezesha shughuli za kijamii na kiuchumi kuendelea kustawi.








MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
KARIBU MKOA WA TANGA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

# MHE. BALOZI OMAR AHIMIZA WENYE MAHITAJI MAALUMU KUCHANGAMKIA ZABUNI ZA SERIKALI KUPITIA NeST



Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), ametoa wito kwa wananchi wenye mahitaji maalumu kuchangamkia fursa za kuomba zabuni za Serikali kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST), kwa kuwa Serikali imetenga asilimia 30 ya zabuni za umma kwa makundi maalum ili kuongeza ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi na kuchochea maendeleo jumuishi nchini.

Alisema hayo wakati wa Hafla ya Kugawa Miguu Bandia kwa watu wenye mahitaji maalumu, iliyoratibiwa na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga Mhe. Mwanaisha Ulenge, pamoja na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Ng'arisha Maisha, iliyofanyika katika Ukumbi wa Regal Naivera, jijini Tanga.

Mhe. Balozi Omar alisema Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki kupitia Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma zinazolenga kuwawezesha wazawa pamoja na makundi maalum kushiriki kikamilifu katika zabuni za Serikali, akibainisha kuwa zabuni zenye thamani ya hadi shilingi bilioni 50 hutangazwa ndani ya nchi ili kuwapa kipaumbele wazawa, huku hata zabuni zinazotangazwa kimataifa zikiendelea kutenga asilimia 30 kwa

kwa makundi hayo.

Alisisitiza kuwa wananchi wenye mahitaji maalumu wanapaswa kuutumia kikamilifu Mfumo wa NeST kuomba zabuni za Serikali katika maeneo mbalimbali ikiwemo usambazaji wa bidhaa, utoaji wa huduma na kazi za ujenzi, badala ya kuziacha fursa hizo zipite, akieleza kuwa Serikali imeweka mifumo na sera zinazolenga kuwainua kiuchumi na kuongeza ushiriki wao katika maendeleo ya taifa.



*Nawahimiza vijana, wanawake na makundi mengine maalum kuendelea kujijengea uwezo na kushiriki katika mafunzo mbalimbali yanayotolewa kuhusu fursa za zabuni za umma ili waweze kushindana na kunufaika na nafasi hizo" alisema Mhe. Balozi Omar*

Akizungumzia msaada wa miguu bandia uliotolewa, Mhe. Balozi Omar amesema vifaa hivyo vitawawezesha walengwa kurejea katika shughuli za uzalishaji na kujitegemea kiuchumi, huku akiwasihi kuvitunza na kuvitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili viwe na manufaa ya kudumu.

Mhe. Balozi Omar alimpongeza Mhe. Mwanaisha Ulenge pamoja na wadau wote waliofanikisha zoezi hilo, akieleza kuwa jitihada za kuwainua wananchi wenye mahitaji maalumu zinapaswa kuungwa mkono na kila mmoja kwa kuwa ni sehemu Muhimu ya maendeleo jumuishi ya Taifa.

*Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kupeleka huduma za maendeleo na kuhakikisha makundi yote ya wananchi yanapata fursa sawa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya nchi" alisema Mhe. Balozi Omar*



Kwa Upande wake Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga Mhe. Mhandisi Mwanaisha Ulenge, aliipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuifanyia tathmini Sheria ya Ununuzi wa Umma ibara 410 ya mwaka 2006, na marekebisho yake ambayo mpaka sasa ina miongo miwili ambayo imetoa fursa kwa makundi mbalimbali hasa vijana, wanawake na makundi maalum.

Mhe. Mhandisi Ulenge, alisema kuwa kwa mujibu wa tafiti iliyofanywa na Trade Mark East Afrika wakishirkiana na Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC) mwaka 2021 ushiriki wa Wanawake ulikuwa 2% tu na makundi mengine ni chini ya hapo, hivyo anaipongeza Serikali kwa kuamua kuifanyia tathmini utekelezaji wa sheria hiyo.










MINISTER
DATE:14TH JULY, 2
-TANGA


IN LOVING MEMORY OF OUR MOTHER
MRS. KAMLESH GUPTA
AIVERA -TANGA


HON. AMB. KHAMIS M. OMAR (MB).
MINISTER
DATE:14TH JULY, 2026 | LOCAT
VERA -TANGA






# SERIKALI ITAENDELEA KUWEKEZA KATIKA MAENDELEO YA PANGANI NA KUBORESHA HUDUMA ZA WANANCHI

Serikali imesema itaendelea kuwekeza katika miradi ya maendeleo na huduma za kijamii ili kuboresha maisha ya wananchi wa Wilaya ya Pangani na Mkoa wa Tanga kwa ujumla.

Hayo yamesemwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), mara baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa ukarabati wa madarasa kumi (10) ya Shule Kongwe ya Msingi Funguni iliyopo Wilaya ya Pangani, Mkoa wa Tanga, ambapo alisisitiza kuwa Serikali haitajikita tu katika kujenga miundombinu mipya, bali pia itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu iliyopo ili idumu na kuendelea kutoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Balozi Omar alisema kuwa majengo ya shule, barabara na miundombinu mingine ya umma yanahitaji matengenezo ya mara kwa mara ili kuzuia uharibifu mkubwa unaoweza kuathiri utoaji wa huduma, akibainisha kuwa ukarabati wa Shule ya Msingi Funguni ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira bora na salama ya kujifunzia.



*Tunawahakikishia wananchi kuwa Serikali itaendelea kuwasikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili kupitia utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla" alisema Balozi Omar*

*Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri katika Mkoa wa Tanga kupitia ujenzi wa barabara, reli na uwanja wa ndege ili kuongeza fursa za biashara, uwekezaji na utalii, na barabara ya Tanga–Pangani–Horohoro ni miongoni mwa miradi muhimu inayounganisha Tanzania na nchi jirani ya Kenya, na kuna umuhimu wa kukamilishwa kwa wakati ili wananchi na wafanyabiashara wanufaike na huduma bora za usafiri na usafirishaji" alisema Mhe. Balozi Omar*

Aidha, Mhe. Balozi Omar alisema ameridhishwa na mafanikio ya miradi mbalimbali ya maendeleo aliyoitembelea katika mkoa wa Tanga, ikiwemo Bandari, ambapo Serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 429 katika uboreshaji wa miundombinu ya bandari hiyo.

Alisema matokeo ya uwekezaji huo tayari yanaonekana, kwani ndani ya kipindi cha Julai mwaka jana hadi Juni mwaka huu, shughuli za kiuchumi zilizofanyika kupitia Bandari ya Tanga zimefikia thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 436, jambo alilosema linaonyesha kuwa uwekezaji wa Serikali unaendelea kuzaa matunda na kuchochea ukuaji wa uchumi





Kwa upande wao, viongozi wa Wilaya ya Pangani wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Muheza ambaye pia alimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Mhe. Ayubu Sebabili, pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Mhe. Sefu Ally Said, walimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuielekezea Pangani rasilimali za maendeleo zilizowezesha kuboreshwa kwa miundombinu ya elimu, barabara na huduma nyingine za kijamii.

Walisema utekelezaji wa miradi hiyo umebadilisha maisha ya wananchi kwa kupunguza changamoto za usafiri na kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu.

Aidha, Viongozi hao pia walimshukuru Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), kwa kutembelea wilaya hiyo na kujionea utekelezaji wa miradi ya maendeleo, wakisema ziara yake imeonyesha dhamira ya Serikali ya kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi.











# WAZIRI WA FEDHA AAGIZA WASTAAFU WAHUDUMIWE KWA HESHIMA

Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), ameiagiza Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na watumishi wa Hazina Ndogo nchini kuhakikisha wanaendelea kutoa huduma bora, zenye heshima, utu na weledi kwa wastaafu wanaolipwa pensheni na Hazina.

Agizo hilo alilitoa alipokuwa akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Hazina Ndogo mkoa wa Tanga wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani humo, ambapo alisisitiza kuwa wastaafu ni kundi muhimu linalostahili kuthaminiwa kutokana na mchango mkubwa walioutoa katika ujenzi wa Taifa walipokuwa watumishi wa umma.

Mhe. Balozi Omar alisema huduma bora kwa wastaafu huongeza ustawi wao na kuimarisha imani ya wananchi kwa Serikali, huku akiwataka watumishi kuwahudumia kwa uvumilivu, kuwapa maelekezo sahihi na kuwasaidia kukamilisha taratibu za uhakiki bila usumbufu usio wa lazima.

Aliwataka pia watumishi kuendelea kutoa elimu kwa wastaafu kuhusu kujihadhari na matapeli wanaojifanya mawakala wa huduma za pensheni, akisisitiza kuwa huduma za pensheni na taratibu za uhakiki hazihitaji mstaafu kutoa fedha kwa mtu binafsi.





Kwa upande wake, Mhasibu Mkuu wa Serikali, CPA Leonard Mkude, ambaye pia ni Msimamizi wa Ofisi za Hazina Ndogo nchini, alimshukuru Waziri wa Fedha kwa kutembelea Ofisi ya Hazina Ndogo Tanga na kuzungumza na watumishi, akisema hatua hiyo imewatia moyo na kuwapa hamasa ya kuendelea kufanya kazi kwa bidii.



CPA Mkude alimshukuru Mhe. Balozi Omar kwa kuwawezesha watumishi kupata ujuzi kupitia mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi, hatua ambayo itaongeza uwezo wao wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aliahidi kuwa watumishi wa Hazina Ndogo Tanga wataendelea kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, uwajibikaji na unyenyekevu mkubwa ili kuhakikisha wananchi, hususan wastaafu wanaolipwa pensheni kupitia Hazina, wanapata huduma stahiki kwa wakati na kwa heshima inayostahili, ikiwa ni kutambua mchango wao mkubwa walioutoa katika kulitumikia Taifa.

Alizungumzia kuhusu huduma zinazotolewa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, CPA Mkude alisema kuwa Hazina Ndogo ni sehemu muhimu ya mfumo wa Serikali katika usimamizi wa fedha za umma nchini. Ofisi hizo zimeanzishwa mahsusi kwa lengo la kusogeza huduma za Hazina karibu na taasisi za Serikali zinazotekeleza bajeti katika ngazi za mikoa, na hivyo kuongeza ufanisi, uwajibikaji, uwazi na nidhamu ya fedha katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali.

Alisema kuwa kwa sasa, Ofisi za Hazina Ndogo zipo katika mikoa yote 25 ya Tanzania Bara, na zote zinafanya kazi chini ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Kupitia Ofisi hizi, Serikali imeweza kuimarisha usimamizi wa mapato, matumizi, malipo ya Serikali, usuluhishi wa hesabu za kibenki, pamoja na usimamizi wa pensheni na mafao mengine yanayolipwa kupitia Hazina.





# SERIKALI KUIFUNGUA TANGA KIUCHUMI KWA MIRADI MUHIMU YA KIMKAKATI

Serikali imeahidi kuendelea kuimarisha uwekezaji katika miundombinu ya kimkakati mkoani Tanga ili kuufungua mkoa huo kiuchumi na kurejesha hadhi yake ya kuwa kitovu cha viwanda nchini.

Ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa Fedha, Mhe. Khamis Mussa Omar (Mb), alipokutana na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Tanga baada ya kuhitimisha ziara yake ya kikazi mkoani humo.

Mhe. Balozi Omar alisema kuwa Serikali inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo upanuzi wa Bandari ya Tanga, uboreshaji wa Uwanja wa Ndege wa Tanga, ujenzi wa barabara pamoja na reli ya kisasa (SGR), hatua ambazo zitaongeza fursa za ajira, biashara na uwekezaji.

Alisema Serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 429 katika upanuzi wa Bandari ya Tanga, ambapo uwezo wa Bandari hiyo umeongezeka kwa kiwango kikubwa na tayari imeanza kuhudumia meli kubwa zinazobeba shehena na makontena mengi zaidi.

*Wananchi wa Tanga wanaanza kuona matokeo ya uwekezaji huu. Bandari imepanuliwa kwa kiwango kikubwa na uwezo wake umeongezeka maradufu. Hii ni hatua muhimu katika kuifungua Tanga kiuchumi," alisema Mhe. Balozi Omar*









Aliongeza kuwa Serikali imejipanga kuhakikisha mradi wa reli ya Tanga-Arusha-Musoma unatekelezwa kwa mujibu wa mipango, huku ikiendelea kuboresha mtandao wa barabara unaounganisha Tanga na mikoa mingine pamoja na nchi jirani ili kurahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa.

Aidha, alisema Serikali itafanya tathmini ya kina kuhusu kuchelewa kwa ujenzi wa barabara ya Tanga–Pangani na kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

Mhe. Balozi Omar alisema maoni na changamoto zilizokusanywa kutoka kwa wananchi na viongozi wa Mkoa wa Tanga zitawasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi, akisisitiza kuwa Serikali

imejipanga kuhakikisha ahadi zote zinazotolewa kwa wananchi zinatekelezwa kwa vitendo.

Kwa upande wake, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (MNEC), Mohammed Salim, alimshukuru Waziri wa Fedha kwa kutembelea Mkoa wa Tanga, alisema ziara hiyo imeongeza hamasa ya kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aliahidi kuwa Chama kitaendelea kuhamasisha wananchi kutumia fursa za kiuchumi na kushirikiana na Serikali katika kusukuma mbele maendeleo ya mkoa huo, huku akisisitiza umuhimu wa kuharakisha utekelezaji wa miradi ya barabara, reli, bandari na miundombinu mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

Amemshukuru Waziri wa Fedha, Mhe. Khamis Mussa Omar kwa kuwa ujio wake katika Ofisi za CCM Mkoa wa Tanga ni heshima kubwa kwa Ofisi hiyo lakini pia kwa Wanachama wake kwa kuwa Chama kinawajibu wa kuisimamia Serikali na usimamizi imara wa miradi ya maendeleo inakifanya Chama kuimarika zaidi.







# MHE. BALOZI OMAR AWAASA TFF KUJENGA VIJANA WENYE MAADILI



Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, ametoa rai kwa wasimamizi na viongozi wa Kituo cha Michezo cha Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) cha Mnyanjani, kilichoko mkoani Tanga, kuhakikisha kuwa, pamoja na kukuza vipaji vya soka, wanajenga kizazi cha vijana wenye maadili, nidhamu na elimu, ili kuwaandaa kuwa wanamichezo mahiri wa sasa na baadae.

Balozi Omar alitoa rai hiyo alipotembelea kituo hicho na kufanya mazungumzo na Meneja wa Oparesheni wa Kituo, Kassim Haji, pamoja na Kocha wa Vipaji kutoka Uingereza, Edwanly Monnely, ambapo alipata fursa ya kujionea maendeleo ya programu za ukuzaji vipaji vinavyoendeshwa na kituo hicho.

Alisema kuwa mataifa mengi duniani yamefanikiwa kuibua vipaji vya hali ya juu kupitia uwekezaji mkubwa katika michezo, lakini baadhi ya wanamichezo walishindwa kufikia mafanikio yaliyokusudiwa kutokana na kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vingine vinavyokwenda kinyume na maadili ya michezo.

“

*Ni muhimu kuwalea vijana katika misingi ya maadili sambamba na kuwanoa kimichezo ili waweze kufanikiwa ndani na nje ya uwanja," alisema Balozi Omar.*



Alisisitiza kuwa nidhamu na maadili ni nguzo muhimu katika kumjenga mwanamichezo bora, akieleza kuwa mafanikio ya kweli katika soka hayaishii uwanjani pekee, bali yanahitaji pia tabia njema na uwezo wa kufanya maamuzi sahihi katika maisha.

Aidha, Balozi Omar alisisitiza umuhimu wa vijana wanaopatiwa mafunzo ya soka kuendelea na elimu ya darasani, akieleza kuwa elimu huongeza upeo wa fikra, huimarisha nidhamu na huwapa uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali hata baada ya kumaliza maisha yao ya uchezaji.

Alibainisha kuwa mchanganyiko wa elimu, maadili na mafunzo bora ya michezo ndiyo msingi wa kuzalisha wachezaji wenye mafanikio endelevu watakaoweza kupeperusha vyema Bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa.



















# WAZIRI WA FEDHA ATEMBELEA KAMPUNI YA BURHAN FURNITURE AHIMIZA KUYAFIKIA MASOKO

Waziri wa Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar (Mb), ametembelea Kampuni ya kutengeneza samani ya Burhan Furniture iliyopo jijini Tanga na kuwataka wamiliki wa kampuni hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kukuza biashara yao, kuifikisha katika masoko ya kimataifa na kuchangia kuongeza fursa za ajira pamoja na mapato ya Serikali.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mhe. Balozi Omar alisema Serikali inaendelea kuthamini mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa, hivyo akawasisitiza wawekezaji kuendelea kuimarisha uzalishaji, kuongeza ubora wa bidhaa na kutumia fursa zilizopo ili kufikia masoko ya ndani na nje ya nchi.

Aidha, aliwataka viongozi na wamiliki wa Burhan Furniture kuendelea kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa uaminifu, akieleza kuwa mapato ya kodi ndiyo msingi



wa Serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na huduma za kijamii.





*Niwapongeze kwa uwekezaji  wenu na mchango wenu katika kutoa ajira kwa Watanzania. Endeleeni kufanya kazi kwa bidii, kuboresha uzalishaji na kulipa kodi kwa uaminifu ili muendelee kuwa sehemu ya maendeleo ya Taifa letu," alisema Mhe. Balozi Omar*

Kwa upande wao, viongozi wa Burhan Furniture walimshukuru Waziri wa Fedha kwa kutembelea Kampuni yao na kueleza kuwa wataendelea kushirikiana na Serikali katika kuendeleza uwekezaji, kuzingatia sheria za kodi na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini.

Limetolewa na
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Fedha
Mji wa Serikali-Mtumba
Mtaa wa Hazina
S.L.P 2802, 40468 Dodoma, Tanzania

Toleo Maalum
ISSN: 3108-8597

ISSN 3108-8597
9 773108 859009